**Muhtasari wa mbinu ya utafiti ya udadisi:**
**Tathmini ya kimataifa ya umuhimu wa matumizi ya Maarifa Asilia (Indigenous Knowledge – IK) katika kukabiliana na mabadiliko ya mazingira.**

***Makala yametafsiriwa na: Mary P. Kiteme, BEd Arts (Kiswahili), UoN***
***Shule Ya Upili ya Inoro, Nanyuki - Kenya.***

***Translation by Mary P. Kiteme, BEd Arts (Kiswahili), UoN***
***Inoro Secondary School, Nanyuki - Kenya.***

Kunayo malengo mawili ya mbinu hii ya utafiti ya udadisi: 1) Kuweza kupata matokeo ya utafiti wa sasa wa matumizi ya Maarifa Asilia (IK) katika kukabiliana na mabadiliko ya mazingira; na 2) Kutathmini iwapo mikakati iliyowekwa inaweza kutumika kuwaleta pamoja washikadau kutoka maeneo mbalimbali ili kubadilishana tajriba yao na mitindo ya usimamizi. Muhtasari wa matokeo ya ripoti kutoka Kenya na Nigeria ni kama ufuatao: (Kwa habari zaidi angalia: sharingknowledge.net.au)

Ingawa umuhimu wa matumizi ya Maarifa Asilia (IK) ya kiafrika katika kuafikia maendeleo-endelevu unaendelea kukubalika na wengi, kuwepo kwa Maarifa Asilia kumeendelea kukutana na matatizo si haba, baadhi yake ikiwepo ukosefu wa mbinu bora za kusambaza na kutumia ujuzi huu.

Njia mwafaka ya kuwasilisha maarifa haya barani Afrika ni kupitia kwa mdomo, kutoka kizazi kimoja hadi kingine; njia ambayo inakumbana na changamoto kubwa kutokana na mabadiliko ya miundo ya jamii katika jamii nyingi za Afrika – zikiwepo uhamiaji wa watu kutoka maeneo ya vijijini hadi mijini, kuathiriwa na utamaduni wa kimagharibi na ile hali ya kudidimia kwa utangamano na mazingira.

## KENYA

1.) Nchini Kenya, uchunguzi wa kina ulifanywa na mashirika mawili, nayo ni Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa (Kenya Meteorological Department – KMD), ambayo ni idara ya serikali na shirika lisilo la serikali nchini lijulikanalo kama “Milirubushi Organisation of Kenya” (MIBOK). Ujumbe pia ulikusanywa kutoka kwa wakazi wa mashinani.

Mashirika ya serikali, mashirika yasiyo ya serikali na watu binafsi hutambua mabadiliko katika mazingira na tabia-nchi (climate change) kupitia njia kadha wa kadha. Hizi ni pamoja na mvua isioyotegemewa, kukauka kwa mito ambayo mbeleni haikukauka, mabadiliko ya mara kwa mara na ya kina zaidi ya tabia-nchi kuliko hapo awali, mavuno duni, kudidimia kwa bio-anuai (bio-diversity) na mmomonyoko wa udongo kutokana na matumizi mabaya ya ardhi miongoni mwa mengine.

Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa ndilo shirika muhimu nchini Kenya ambalo hujihusisha na kukusanya na kuhifadhi taarifa zinanohusu hali ya hewa na kuzingatia mabadiliko katika hali ya hewa na tabia-nchi. Hoja yao kubwa inaweza kujumuishwa chini ya uhifadhi wa habari muhimu kuhusu tabia-nchi, tofauti na mabadiliko katika tabia-nchi na njia za kukabiliana na maafa. Yale mawili ya kwanza yana uhusiano wa moja kwa moja na Maarifa Asilia (IK) nalo la mwisho linahusiana na matokeo ya tofauti na mabadiliko ya tabia-nchi, kama vile ukame na madhara yake. Shughuli za idara hii zinahusiana na uchambuzi wa habari muhimu kuhusu tabia-nchi za muda mrefu ili kuona kana kwamba kunayo mienendo maalum na sababu ya mienendo hiyo. Vilevile, huwafahamisha wananchi kuhusu mabadiliko ya tabia-nchi kupitia vyombo mbalimbali vya mawasiliano na pia kuwazindua kwa kurejelea matukio mageni ambayo hayakuonekana hapo awali. Kwa mfano, ilikuwa ni nadra sana kuwaona mbu katika maeneo ya Nairobi na Nyanda za Juu katikati mwa nchi lakini sasa ni tukio la kawaida. Habari kama hizi huwazindua watu na basi huweza kueleza sababu za kubuni njia za kukabiliana na matukio kama hayo.

Kwa mujibu wa afisa mmoja wa Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa, wale wanaofaa zaidi kuutekeleza mpango huu wa kuwasilisha ujumbe huo mashinani ni pamoja na maafisa wa serikali na viongozi katika jamii wakishirikiana na wanasayansi. Shughuli za kutumia Maarifa Asilia (IK) zinazoendelezwa na shirika hili la KMD katika jamii ni pamoja na utabiri wa mara kwa mara wa hali ya hewa na juhudi za kujaribu kuelewa Maarifa Asilia na kutoa maelezo ya kisayansi. Sababu ya kuhusisha Maarifa Asilia mashinani ni kuwa ndiyo inayoeleweka zaidi na wanajamii. Inabidi basi kuuelewa utamaduni wao kabla ya kuleta mabadiliko yoyote na hivyo basi itakuwa rahisi zaidi ikiwa shughuli hizo zinamilikiwa na jamii.

Inatambulika sasa kwamba ukuzaji wa IK una misingi ya kisayansi. Viongozi na watawala wa mashinani wanaoyamiliki yale Maarifa Asilia na wanaoheshimika sana katika jamii wanatekeleza matumizi ya Maarifa Asilia. Ili kupanua zaidi matumizi na kukubalika kwa Maarifa Asilia, ingefaa kwanza ujumbe uliomo uratibiwe rasmi, kisha itafutwe namna ya kuupokezana kutoka kizazi hadi kingine na pia kushughulikia rasilmali zinazohitajika kuutekeleza mpango huo.

Shirika lisilo la kiserikali la MIBOK hufanya kazi pamoja na mashirika yaliyo nyanjani na mashule ili kudumisha uhifadhi wa bio-anuai, kutafuta njia za kukabiliana na kemikali na njia za utupaji wa taka, na pia kutafuta mbinu za kukabiliana na kuenea kwa janga la UKIMWI. Shughuli zake za kudumisha uhifadhi wa bio-anuai zinahusika moja kwa moja na Maarifa Asilia na mabadiliko katika tabia-nchi. Ili kufanikisha Maarifa Asilia katika kukabiliana na hali ya mazingira na mabadiliko katika tabia-nchi, MIBOK inahitaji kuungwa mkono kwa njia ya ufadhili wa shughuli zao. Hizi ni pamoja na kuanzisha miche, kupanda na kuitunza miti.

Wakulima wengi wanadai kuwa mafanikio ya matumizi ya Maarifa Asilia yatatokana na wakulima wenyewe kutumia Maarifa Asilia katika mashamba yao. Ingekuwa ni kielelezo bora ili wengine waweze kuwaiga. Wakulima wako tayari kushiriki katika kuutekeleza ikiwa wangepata miche ya miti ya asili ambayo inaweza kustahimili hali ya hewa katika maeneo yao. Vilevile, ingefaa kama wangepata miche ya miti ya kigeni ili washirikishe yale Maarifa Asilia katika kilimo chao.

Inaripotiwa pia kwamba kama watu wangeelimishwa na kuzinduliwa kuhusu Maarifa Asilia, ingefaa sana ili kuboresha utekelezaji wa teknolojia hii. Hata hivyo, MIBOK inapendelea washikadau wote washirikishwe ili njia mwafaka na kubadilishana ujumbe kuhusu teknolojia hii ziweze kufikiwa. Wanapendekeza kwamba vikundi ambavyo vingependa kutekeleza vipengele fulani vya utaratibu huu vifadhiliwe na kumotishwa. Uanzilishi wa shughuli zinazoenda sambamba na upandaji wa miti (kama vile ufugaji wa nyuki) unaweza kuwahimiza wakulima wengi na watu binafsi kupanda miti katika mashamba yao.

Vizingiti vilivyotambuliwa vinavyozuia mafanikio katika kukabiliana na mabadiliko katikia mazingira vilihusu mambo kama i) Ongezeko la watu; ii) Uharibifu wa mazingira; iii) Kukosa ujuzi mashinani; na iv) Mapuuza katika baadhi ya watu (hasa vijana). Kwa mfano; watu wengi wanaamini ya kwamba Maarifa Asilia huenda yasifanye kazi na ni ya kale, yaliyopitwa na wakati na yasiyofaa. Pia kuna kutopatikana kwa ujumbe kwa urahisi katika kiwango cha mashinani na huenda watu wakakosa kujua mashirika yanayojihusisha na ukuzaji wa Maarifa Asilia, umaskini na utabiri wa hali ya anga usioweza kutegemewa.

Utafiti huu mdogo wa matumizi ya Maarifa Asilia katika kukabiliana na mazingira na mabadiliko ya tabia-nchi umeonyesha kwamba katika viwango vyote (Kitaifa, wilayani na mashinani) wahusika wanatambua kuwepo kwa mabadiliko katika mazingira na tofauti katika tabia-nchi. Hata hivyo, tashwishi zingalipo kuhusiana na kuaminika kwa Maarifa Asilia. Kwa vile Maarifa Asilia sio maarifa ya kijumla, kutambuliwa kwa wenye ujuzi wa Maarifa Asilia na maeneo inakotumika ni jambo la kutiliwa maanani. Utafiti huu umeonyesha kwamba hatua ya kwanza ya kuyaelewa Maarifa Asilia ni kuyaratibisha na kuyafanya yaweze kufikia umma.

2.) Bali na kukubaliana kuhusu umuhimu wa kubadilishana ujumbe unaohusiana na Maarifa Asilia na watu wengine, afisa wa Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa hakuona haja ya kongamano la kimataifa linaloleta pamoja wahusika mbalimbali kujadiliana masuala hayo kama njia bora ya kukabiliana na hali ya mazingira na mabadiliko ya tabia-nchi mashinani.

Afisa huyo alitambua kwamba masuala hayo yamefafanuliwa wazi kupitia kamati inayoshughulikia mabadiliko ya tabia-nchi (IPCC) na kilichobaki ni kuyateremsha mashinani. Alipendekeza kuwa jambo hili lingeshughulikiwa vyema zaidi kupitia juhudi za kiserikali.

Afisa wa MIBOK kwa upande wake aliona haja ya kongamano la kimataifa linaloleta pamoja wataalamu kujadili njia mwafaka za kuleta uwiano na kukabiliana na mabadiliko ya mazingira na tabia-nchi. Hii itawawezesha kushirikisha maoni ya wengine kuhusu jambo hilo, hivyo basi kuwafanya wakubali matumizi ya Maarifa Asilia.

Faida za kushirikisha mikakati iliyopo kuhusu Marifa Asilia kutoka kwa wahusika wengine ilitambuliwa. Baadhi yake ni kuwa, kwa kuja pamoja, wahusika watahamasishana na kuhimizana kuhusu matumizi ya Maarifa Asilia, jambo ambalo litasaidia katika kukabiliana na ile hali ya Maarifa Asilia kuhusishwa na mambo ya zamani yaliyopitwa na wakati. Kufanya kazi pamoja na kwa ushirikiano na vikundi vingine husika na kubadilishana maoni kuhusu matumizi ya Maarifa Asilia kitaifa na kimataifa kutakuwa ni hatua kubwa katika kukubalika na kutumika kwa mbinu za Maarifa Asilia na kuhakikisha ya kwamba wengine wamefikiwa na ujumbe huo kote ulimwenguni. Kubadilishana maarifa mapya kutafaa sana kwani Maarifa Asilia yataweza kuratibiwa, kutathminiwa na kutumika katika upeo mpana; jamii nyinginezo zaweza kuwa zina Maarifa Asilia yanayohusiana na mabadiliko katika tabia-nchi na jambo hili litapanua upeo wa ujuzi katika Maarifa-Asilia.

**NIGERIA**

1.) Nchini Nigeria, taarifa zinazohusiana na matumizi ya Maarifa Asilia (IK) zilikusanywa kutoka kwa wawakilishi kutoka kituo kijulikanacho kama “Centre for Arid Zone Studies, Maiduguri, The National Meteorological Agency, Abuja” na “Centre for Environmental Resources and Hazards Research” Chuo Kikuu cha Jos na pia kutoka kwa wahojiwa kutoka vijiji vitatu katika eneo la Bornu State.

Waliohojiwa kutoka vijijini, watafiti na mashirika ya kiserikali walitambua kupungua katika bio-anuai (bio-diversity), ongezeko la kuenea kwa jangwa, ukataji wa misitu, mmomonyoko wa udongo, upungufu wa mvua, mabadiliko makubwa katika nyakati mvua hiyo inatarajiwa, muda mrefu unaochukuliwa na maji yachimbwayo kutoka chini kutosha, kukawia kwa mito kujaa maji, ukame wa mara kwa mara, upungufu wa malisho, mavuno duni na kukauka kwa chemichemi kama ishara za mabadiliko ya mazingira na tabia-nchi.

Mabadiliko ya mara kwa mara ya tabia-nchi pamoja na panda-shuka katika kiwango cha mvua na tofauti za kiwango cha mvua kulingana na maeneo ndicho chanzo cha shughuli za kila siku kwa wakazi wa Nigeria Sahel. Jambo hili limechangia pakubwa katika kupungua kwa malisho, uhaba mkubwa wa maji na ongezeko la magonjwa ya mifugo na mimea.

Maarifa Asilia ya wakazi waliohojiwa kuhusiana na mienendo ya mvua yangelinganishwa na maarifa ya kisayansi. Mienendo ya kutokea kwa ukame kama ilivyoelezewa na wakazi na mienendo ya mvua kwa mujibu wa matokeo ya uchunguzi wa kisayansi ilitoa matokeo yanayolingana. Kabla ya mabadiliko makubwa katika hali ya tabia-nchi, wafugaji wengi wa kuhamahama waliashiria kuhama kama njia bora zaidi ya kukabiliana na ukosefu wa malisho katika sehemu ya kusini humo nchini na kurejea sehemu ya kaskazini pindi tu mvua irudipo.

Baadhi ya mbinu za Maarifa Asilia wanazotumia wakazi hao ili kutafuta suluhisho la kukabiliana na mabadiliko katika mazingira na tabia-nchi ni kama zifuatazo: Kupanda mimea inayostahimili ukame; kupanda mimea inayokomaa kwa haraka; kupanda mimea inayotoa mavuno marudufu; kupanda mimea isiyohitaji pembejeo nyingi; kupanda mimea ya kunyunyiziwa maji; kupanda mimea na kuweka mifugo anuai; kurudia upanzi; kuzingatia mienendo ya mifugo; kubadilisha hali ya maisha badala ya kuhamahama ili waweze kusaidiwa; kupunguza idadi ya mifugo; kuhamisha ujira; kuuza baadhi ya mali zao; na kubuni mbinu za kuhifadhi maji na chakula.

Mashirika mengi hutenda kazi katika miundo maalum ya mazingira. Hata hivyo, mengi kati ya mashirika hayo hayajatumia Maarifa Asilia katika kushughulikia masuala ya mabadiliko katika mazingira na tabia-nchi. Wahojiwa wengi walipendekeza kwamba Maarifa Asilia yanaweza

kuonanishwa na mipango ya mashirika hayo pasi na kubadilisha utaratibu uliyowekwa na mashirika ya kiserikali bali shughuli zao ziweze kutangamanishwa.

2.) Kuboresha njia za kufikia wakazi mashinani ilionekana kama njia bora kuliko kuandaa mkutano wa kimataifa unaowaleta pamoja wahusika mbalimbali ili kujadiliana kuhusu njia bora zaidi za kukabiliana na mabadiliko ya mazingira na tabia-nchi kupitia mbinu ya Maarifa-Asilia. Wahusika wengi kutoka mashirika mengi wanapendekeza kwamba Maarifa Asilia yanaweza kuoanishwa na baadhi ya mipango ya shughuli zao bila kuingilia sana hali ambayo imedumishwa na mashirika ya kiserikali.

Wanaonelea kwamba kuoanisha vipengele fulani vya Maarifa Asilia kunaweza kufufua shughuli za Maafisa-nyanjani wa kilimo. Vilevile, wanapendekeza kuwepo kwa huduma za madaktari wa mifugo wa kuhamahama kuambatana na njia zinazofuatwa na wafugaji wa kuhamahama, au madaktari hao wafungue kliniki zao katika maeneo maalum ili kuwahudumia wafugaji hao, kwa vile kuhamahama ni njia muhimu na ya kitamaduni ya kutafuta suluhisho la uhaba wa malisho.